# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA MKOA WA MTWARA
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Mtwara na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 - Aprili, 2022) kwa mkoa wa Mtwara. **(b)** Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za Msimu katika sehemu mbalimbali za mkoa wa Mtwara. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Novemba hadi Aprili, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo.**

- *Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Mtwara.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu.*

**Mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022)**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya mkoa wa Mtwara. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili Novemba, 2021 na zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022. Aidha, upo uwezekano wa kutokea kwa mgandamizo mdogo wa hewa kaskazini mwa kisiwa cha Madagascar hivyo kusababisha kurejea kwa mvua katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Mtwara mwishoni mwa mwezi wa Aprili, 2022.

***Angalizo:***

*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA MTWARA
**Umetolewa: 27/10/2021**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Mtwara.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Mtwara, Mtwara.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Mtwara.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo cha bustani.*
- *Mamlaka husika na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na viwandani.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021- Aprili, 2022) kwa wilaya ya Mtwara

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba-Aprili kwa wilaya ya Mtwara ni milimita 1000 hadi 1040.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Novemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani.
- Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua maji na hata kukauka kwa visima, hususan vile vifupi.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga.
- Wakulima na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji.


Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**
*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**




**Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA MASASI
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Masasi.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Masasi, Mtwara.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Masasi.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Mamlaka husika na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na viwandani.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021- Aprili, 2022) kwa wilaya ya Masasi

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba-Aprili kwa wilaya ya Masasi ni milimita 880 hadi 1000.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Novemba, 2021.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani.
- Vipindi vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua maji na hata kukauka kwa visima, hususan vile vifupi.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga.
- Wakulima na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA NEWALA
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Newala.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Newala, Mtwara.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Newala.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Mamlaka husika na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na viwandani.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021- Aprili, 2022) kwa wilaya ya Newala

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba-Aprili kwa wilaya ya Newala ni milimita 960 hadi 1000.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Novemba, 2021.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

**Angalizo:**

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani.
- Vipindi virefu vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua maji na hata kukauka kwa visima, hususan vile vifupi.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga.
- Wakulima na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA TANDAHIMBA
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Tandahimba.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Tandahimba, Mtwara.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Tandahimba.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo cha bustani.*
- *Mamlaka husika na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na viwandani.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021- Aprili, 2022) kwa wilaya ya Tandahimba.

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba-Aprili kwa wilaya ya Tandahimba ni milimita 960 hadi 1040.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Novemba, 2021.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani.
- Vipindi virefu vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua maji na hata kukauka kwa visima, hususan vile vifupi.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga.
- Wakulima na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji.

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2021 – APRILI, 2022) KWA WILAYA YA NANYUMBU
## Umetolewa: 27/10/2021

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za msimu katika kipindi cha Novemba, 2021 hadi Aprili, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Nanyumbu.




Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2021 – Aprili, 2022) kwa wilaya ya Nanyumbu, Mtwara.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Nanyumbu.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.*
- *Wakulima wanashauriwa kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo cha bustani.*
- *Mamlaka husika na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na viwandani.*

### Mvua za Msimu (Novemba, 2021- Aprili, 2022) kwa wilaya ya Nanyumbu.

**Zitaanza:** Wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Zitaisha:** Wiki ya pili ya mwezi Aprili, 2022.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Novemba-Aprili kwa wilaya ya Nanyumbu ni kati ya milimita 840 hadi 1000.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Novemba, 2021.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano mkubwa wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku 10 au zaidi katika msimu huu.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Msimu uliopita.

**Angalizo:**

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

- Maeneo ya kutuamisha maji yatapungua na kuruhusu kilimo cha bustani.
- Vipindi virefu vya ukavu vinaweza kupelekea kupungua maji na hata kukauka kwa visima, hususan vile vifupi.

#### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kulima kilimo cha bustani kama vile mbogamboga.
- Wakulima na wananchi kwa ujumla wanashauriwa kutumia teknolojia za uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.
- Mamlaka za maji zinashauriwa kujiandaa na uwezekano wa upungufu wa maji.


Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**
*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*105A – 09/19*

**Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**